

MAAGIZO YA CHUO - BUSOKELO DVTC

Zingatia: Mwanachuo aliyechaguliwa KUSOMA KUTWA atapaswa alipie fedha yote kupitia control number utakayopata chuoni, fedha taslimu (cash) hazitapokelewa.

NA	MAHITAJI	GHARAMA		
		UMEME	USEREMALA	USHONAJI
1	Suruali mbili (2)	50,000.00	50,000.00	50,000.00
2	Ovaroli moja(1) bluu kwa wanachuo wote(isipokua fani ya ushonaji)	30,000.00	30,000.00	-
3	Fulana ya VETA	20,000.00	20,000.00	20,000.00
4	Nembo mbili za VETA	3,500.00	3,500.00	3,500.00
5	Fedha za michezo	30,000.00	30,000.00	30,000.00
6	Fedha za kitambulisho	7,500.00	7,500.00	7,500.00
7	Fedha za tahadhari	10,000.00	10,000.00	10,000.00
8	Ada ya mafunzo kwa wanachuo wa kutwa kwa mwaka ni Tsh.60,000/=, kwa muhula ni 30,000/=	30,000.00	30,000.00	30,000.00
JUMLA		181,000.00	181,000.00	151,000.00

MUHIMU:

- KWA MUHULA WA KWANZA, MWANAFUNZI ANAPASWA KULIPA FEDHA YOTE ILIYOAINISHWA KWENYE JEDWALI MARA TU ANAPORIPOTI CHUONI KWA MARA YA KWANZA.
- MUHULA WA PILI MWANAFUNZI ATALIPIA ADA SHILINGI ELFU THELATHINI (30,000/=) NA FEDHA YA MTHANI WA TAIFA KIASI CHA SHILINGI ELFU ISHIRINI NA TANO (25,000/=)
- KILA MWANAFUNZI ANATAKIWA KUWA NA BIMA YA AFYA AMBAYO NI YA TAIFA. ALIYE NA BIMA YA TAIFA AJE NA KADI. ASIYE NA BIMA YA AFYA YA TAIFA ATAPASWA KULIPIA SH. 50,400/- KUPITIA NAMBA YA MALIPO (CONTROL NUMBER) ITAKAYOTOLEWA NA MFUKO WA BIMA YA AFYA YA TAIFA. HAKIKISHA UNA CHETI CHA KUZALIWA NA WALIO NA UMRI ZAIDI YA MIAKA 18 ANAPASWA KUWA NA NIDA NAMBA.

2. Mwanachuo anatakiwa kununua vifaa vifuatavyo kwa matumizi yake binafsi awapo chuoni:

- Mashati mawili meupe (mikono mifupi ya tetroni)
- Sweta moja la bluu iliyokolea (uzi wa sweta umeambatanishwa kwenye barua hii).
- Jozi moja ya viatu vyeusi vya ngozi, vya kufunga kamba visigino vifupi na soksi nyeusi zenye urefu wa kawaida.
- Mkanda mweusi wa ngozi
- Wanachuo wa useremala na umeme waje na viatu vya karakana (industrial boots) na zitakaguliwa
- Daftari kubwa (10) kwa wote
- Mkebe (mathematical set) pamoja na kikokotoo (Scientific Culculator)
- Drawing pencil (kalamu ya penseli ya kuchorea) kwa wote
- Karatasi nyeupe A4 (VISTA PLUS) AU (NOPA) ream moja kwa kila mwaka(ni muhimu sana kwa ajili ya matumizi yako ya darasani) kwa wanachuo wote.
- Unatakiwa uje na Tsh. 3,000/= ya picha (2) za paspoti size kwa ajili ya kumbukumbu za ofisi na faili la mwanachuo. Picha utapigwa hapa hapa chuoni.
- Wanachuo wote wanapaswa kuja na kwanja pamoja na jembe lenye mpini wake.
- Mwanachuo atapaswa kuhudhuria mafunzo kwa vitendo awapo mwaka wa pili kwa muda wa wiki nane(8), hivyo mzazi anapaswa kulipia malazi na chakula kwa kipindi chote awapo katika mafunzo.
- Wanachuo hatapokelewa chuoni iwapo atafika bila kutekeleza vifungu vyote vilivyotajwa hapo juu.
- Mwanachuo unatakiwa kufuata sheria na taratibu zote za chuo zilizo ambatanishwa kwenye barua hii.
- Wanachuo wote wanatakiwa kufika chuoni na barua hii siku ya kuripoti kabla ya saa 9:30 alasiri kwa siku za kazi.

MAELEKEZO MENGINE UTAPEWA UFIKAPO CHUONI .

Nakutakia maandalizi mema.

KARIBU SANA.

MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI



FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

a) MWANACHUO

Mimi ninakubali nafasi ya mafunzo katika fani niliyopangiwa pamoja na kuzingatia sheria na taratibu za chuo ambazo nimezisoma na kuelewa vizuri.

Saini..... Tarehe.....

b) MZAZI / MLEZI/MDHAMINI

Mimi..... ambaye ni mzazi / Mlezi mdhaminiwa mtajwa hapo juu nathibitisha kuwa nitamdhmini na nitamlipia gharama zote za mafunzo ikiwa ni ada na michango mingine wakati wote wa mafunzo kama ilivyoelezwa katika fomu ya kuniunga na chuo.

Saini Tarehe.....

Namba ya simu.....